

MAKAO MAKUU

Ghorofa ya 4, Jengo la PSSSF, Barabara ya Makole
S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua pepe: info@ewura.go.tz

Tovuti: <http://www.ewura.go.tz>

TANGAZO KWA UMMA

MWITO WA MAONI YA WADAU KUHUSU MAOMBI YA MAREKEBISHO YA BEI ZA MAJI KUTOKA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA YA IGUNGA (IGUNGA WSSA) KWA MWAKA 2020/21 – 2022/23

Maombi ya Mabadiliko ya Bei Na. TR-W-19-002

Mnamo tarehe 6 Februari 2020 Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ilipokea maombi kutoka Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira ya Igunga (Igunga WSSA) ya kutaka kurekebisha bei za huduma zake za maji safi na usafi wa mazingira kwa mwaka 2020/21 hadi 2022/23. Majedwali namba 1 hadi 3 hapa chini yanaonesha bei na tozo za sasa na bei zinazopendekezwa.

Jedwali Na 1: Bei ya Sasa na Zinazopendekezwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi kwa Uniti moja ya ujazo)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zinayopendekezwa					
	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiliko	2021/22	Mabadiliko	2022/23
Majumbani	1,060	70%	1,805.14	5%	1,895.39	5%	1,990.39
Taasisi	1,390	69%	2,344.50	13%	2,641.72	-2%	2,584.80
Biashara	1,750	53%	2,686.00	5%	2,821.06	5%	2,962.11
Viwanda	1,750	53%	2,686.00	5%	2,821.06	5%	2,962.11
Magati	1,500	7%	1,600.00	5%	1,680.00	5%	1,764.00
Wateja wa Jumla	3,460	7%	3,700.00	0%	3,700.00	8%	4,000.00

Jedwali Na 2: Ada za Sasa na Zinazopendekezwa za Maunganisho Mapya ya Maji (Shilingi/ Maunganisho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa		
	2019/20	2020/21	2021/22	2022/23
Majumbani	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho Mapya	Asilimia 20 ya Maunganisho Mapya		
Taasisi				
Biashara				
Viwanda				
Magati				

Jedwali Na 3: Ada ya Sasa na Zinazopendekezwa za Kurejeshwa Huduma ya Maji (Shilingi/Marejesho)

Kundi la Wateja	Ada ya Sasa	Ada Zinazopendekezwa					
	2019/20	Mabadiliko	2020/21	Mabadiiko	2021/22	Mabadiliko	2022/23
Majumbani	10,000	0%	10,000	50%	15,000	0%	15,000
Taasisi	10,000	0%	10,000	100%	20,000	0%	20,000
Biashara	10,000	0%	10,000	100%	20,000	0%	20,000
Viwanda	10,000	0%	10,000	150%	25,000	0%	25,000

Kwa mujibu wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Igunga sababu kuu ya kuomba marekebisho ya bei za huduma zake ni kuiwezesha Mamlaka kukidhi ongezeko la gharama za uendeshaji na matengenezo kutokana na mradi wa Ziwa Victoria. Bei na tozo zinazopendekezwa na Igunga WSSA zitaiwezesha Mamlaka kulipa gharama za uendeshaji, kuongeza mtandao wa huduma na kufanya uwekezaji katika miundimbinu ya maji na hivyo kuboresha huduma kwa wateja wake.

Kwa mujibu wa kifungu Na. 19 (2) (b) cha Sheria Na. 414, EWURA inakaribisha maoni ya wadau wote kuhusu maombi ya Mamlaka ya Maji Tabora. Wadau wanaopenda kutoa maoni wawasilishe maoni yao kwa njia ya barua pepe kwa anuani ya info@ewura.go.tz wakati wowote tangu tarehe ya Tangazo hili. Maoni kwa njia ya ujumbe wa maandishi au sauti kupitia mtandao wa WhatsApp, ujumbe wa simu ya mkononi yatapokelewa kupitia namba **+255 753 035 876** na **+255 767 201 354** kuanzia tarehe 16 Aprili 2020. Aidha, tarehe hiyohiyo, masanduku ya maoni yatawekwa katika ofisi za Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Igunga na Halmashauri ya Wilaya ya Igunga. Mwisho wa kuwasilisha maoni utakuwa tarehe 27 Aprili 2020.

Maelezo zaidi yanaweza kupatikana katika ofisi za **EWURA KANDA YA KATI, GHOROFA YA TANO, JENGO LA PSSSF; BARABARA YA MAKOLE, DODOMA** au **OFISI ZA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA IGUNGA.**

**Imetolewa na:
MKURUGENZI MKUU**